



Kwa pamoja
tupambane na
janga hili



**Mwongozo wa ukingaji kwa jamii za kiasili indigenous rights radio
Mwongozo wa ukingaji, kituo cha redio cha haki za jamii zaa kiasili
Wakati wa dharura ya janga la covid-19**

Cultural  Survival



Jamii za kiasili zinakabiliana na changamoto ambayo haijawahi kutokea kwa sababu ya covid-19.

Cultural survival wanafanya kazi ya kuunga mkono kituo cha redio cha jamii za kiasili ambayo inaweza kuleta mabadiliko makubwa jinsi jamii za kiasili wanavyoshughulikia tatizo hili.

Redio ya jamii ni chombo chenye nguvu kwa jamii za kiasili, kutekeleza haki zao kwa kujitolea uamuzi, haki ya uhuru wakujiieleza, kuwasilisha habari husika yenye manufaa, na iliyo na umuhimu kwa wanajamii wenyewe.

Maarifa ni nguvu na jamii inawezeshwa kupitia redio.

Galina Angarova
Executive Director
Cultural Survival



Mwongozo mzuri wa mazoezi wa covid-19

Mwongozo huu wa mazoezi kitakuwa chombo cha msaada kwa wanahabari wa jamii za kiasili kwa mawasiliano ili waweze kuchua na kupambana dhidi ya covid-19 katika kazi za kila siku.

Lengo kuu:

kuwezesha vyombo vya mawasiliano kwa wanahabari kutoka jamii za kiasili kushughulikia na kukabiliana na athari za Covid-19.


Hadhira:

Mwongozo huu ni chanzo kwa wafanyakazi wa redio, waandishi wa habari asilia, watangazaji na wanahabari wote ulimwenguni kote kuwa usalama wao wakati wa Covid-19.





COVID-19



Binadamu wanakabiliana na janga jipya linalojulikana kama Covid-19.

Chanjo ya tiba yake bado inafanyiwa kazi.

Serikali ulimwenguni kote zinatumia kanuni zinazopunguza binadamu kutangamana, hali ya uchumi, kisiasa na kijamii imezidi kuwa mbaya.

Dharura hii ya ulimwenguni imepelekea kufikiria juu ya ufahamu wa mababu ambao watu wa asilia wanashikilia na jinsi ya kuboresha uhusiano wetu na ardhi dunia.


Tukuze na kujenga njia zingine za maisha ambazo zinahusisha matumizi ya watu na shughuli za kibinadamu ambazo haziharibu mazingira.



Kwa sasa vyombo vya habari vya jamii za kiasili zinafanya jukumu muhimu. Kwa dharura hii ya usafi wa ulimwengu, wanahabi wanapaswa kutoa taarifa sahihi kwa njia wazi na ya uwajibikaji.


Cultural survival wanaweka mwongozo huu pamoja kwa mwitikio wa dharura, kutambua jukumu la redio na umuhimu na usalama wa wanahabari asilia.

Kumbuka, pendekezo ambalo limesisitizwa ni pamoja na kuepuka mikusanyiko ya watu, kuosha mikono yetu vizuri na utumiaji wa barakoa.



Udhaifu na nguvu

Mabadiliko haya yanaleta fursa ya kuonyesha mazingira magumu na nguvu ya watu wa jamii zaa kiasili.



Afya, maji ya kunywa, dawa



Ukosefu wa upatikanaji wa afya, dawa, maji ya kunywa na taarifa sahihi juu ya kila moja, inaeleweka kama mazingira magumu. Maadili ya jamii, mfumo wa chakula dawa za jadi na ushirika huzingatiwa kama nguvu.

Kutoka Cultural survival tunashiriki mwongozo huu kukabiliana na hali ya dharura kwa kutambua jukumu la redio na umuhimu wake na usalama wa wanahabari wa asilia. Ni mapendekezo ya mazoez ya kuzuia kutumia mawasiliano ya redio wakati wa Covid-19. Lina sehemu mbili Sehemu ya kwanza imeelekezwa katika wanachama wa redio na wafanyakazi




Sehemu ya pili ni mwongozo wa kutoka yaliyomo katika uwajibikaji kwa jamii za kiasili.



Sehemu ya 1

Wafanyakazi wa redio na wakujitolea
Kikoa cha redio inapswa kufanya nini?
Usalama kwanza!





Kuunda mpango wa usalama kwa wanachama wa redio

Ni lazima kufanya hivi kama kikoa, kwa kuzingatia mapendekezo ya shirika la afya duniani, la serikali kuu, la mamlaka ya afya na mamlaka ya serikali za mitaa.

Chambua hatari

Unaposafiri katika jamii hakikisha kufuata hatua zinazochukuliwa na viongozi wa jamii na serikali za mitaa. Hii ndio safu yako ya kwanza ya ulinzi.

Kutambuliwa vizuri

Kama wanachama wa vyombo vya habari vya mawasiliano ili kuzuia tatizo na vizuizi na kanuni zilizopitishwa na kila nchi. Idhini inayofaa inapaswa kuandamana na wafanayakazi ndani na nje ya studio.

Usijihatarishe

Maisha yako ni ya thamanai kuliko vitu vya redio. Usijipeleke mwenyewe katika maeneo hatarishi isipokuwa ukiwa na vifaa kinga vya kutosha, vinginevyo usiende, kumbuka kuwa wanahabari ni binadamu pia.

Rekebisha ugawaji wa kazi inayowazunguka walio katika mazingira magumu

Ikiwa kikoa kimeundwa, na watu wengine wana umri mkubwa sana au kama mtu ana magonjwa sugu, anapaswa kupewa kazi zingine amabazo anaweza kufanyia nyumbani.

Safisha eneo la kazi
kila wakati

Tumia kichungi cha
upepo au sifongo kwa
kipaza sauti

Tumia viuaviini
kusafisha vifaa baada
ya mahojiano

Epuka kuleta watu
zaidi ya wawili kwenye
redio

Kuunda mpango
kupitia utiririshaji
kama chaguo la
kutokwenda kwenye
kibanda cha kurekodi.



Safisha eneo la kazi kila wakati

Tumia pombe ya kioevu katika mkusanyiko wa asilimia 70, pia unaweza kutumia klorini au viuaviini iliyoyeyushwa katika maji.

Kuunda mpango kupitia utiririshaji kama chaguo la kutoenda kwenye kibanda cha kurekodia

Ratibu uunganisho wa kibanda na mtu anayesimamia, hali hii inatoa ubora wa sauti kuliko kupitisha kwa njia ya simu. Ikiwa hauna rasilimali ya kipitisha kwa njia hii, ifanye kwa simu kama chaguo la pili. Unaweza kupata chaguo la utiririshaji wa bure kwenye kiunga kifuatacho:

www.giss.tv

Tumia kichungi cha upepo au sifongo kwa kipaza sauti

Kipaza sauti ni njia ya kuambikiza. Mwisho wa programu ni muhimu kubadilisha sifongo au kuifunika kwa mfuko mpya (plastiki au kitambaa) kwa kila mgeni. Wajibika.

Tumia viuaviini kusafisha vifaa baada ya mahojiano

Unapaswa kutumia kitambaa kilicholowekwa kwenye pombe ethyl. Epuka kusafisha na chlorine kwa sababu ni babuzi itababua vifaa. Unaweza kununua pombe ethyl kwenye madukaa ya dawa.

Epuka kuleta watu zaidi ya wawili kwenye redio

Hii inapaswa kufanywa tu ikiwa ni muhimu sana, zingatia kukaa mbali na kuvaa barakoa.

Sehemu ya pili

Wafanyakazi wa redio na wakujitolea

Katika sehemu hii tunatoa muhtasari wa baadhi ya miongozo iliyotolewa na shirika la afya duniani na tovuti maalum kwa kuzingatia janga la Covid-19, ili jamii za kiasili, wanahabari wanaweza kutoa taarifa kwa njia ya uwajibikajin na sio ya kutisha.

Habari bandia



Epuka habari mbaya na za uongo

Shirika la afya duniani lilitengeneza neno “infodemic” kueleza habari potofu na habari isiyo sahihi ambayo inazunguka katika vyombo vya habari na majukwaa tofauti tofauti. Habari potofu na ya uongo husababisha mkanganyiko na maamuzi mabaya kutoka kwa watu wengi, ambayo inaweza kuwa na athari katika ustawi wa kila mtu. Epuka mada za kutisha na kuchochea.



Zingatia takwimu rasmi na ya kisayansi kuhusu ugonjwa na mapendekezo ya shirika la afya duniani

Kumbuka kuwa wewe sio mtaalam wala mwanasayansi juu ya mada hiyo, kwa hivyo utafiti tu wa wataalam wa afya ya umma, wataalam wa

magojwa mlipuko, wauguzi, waundaji wa chanjo na wataalam wa maumbile wanaweza kuelezea mambo ya kisayansi ya janga hili kulijulisha umma.



World Health Organization



Kukuza dawa za kiasili za mababu

Tuna maarifa juu ya jinsi ya kuimarisha kinga yetu kwa dawa za jadi na vyakula vya asili. Tuwahoji waganga wa jadi na watu wa aina hiyo.




Sambaza taarifa hiyo katika lugha zetu za mama na lugha ya kawaida ya nchi yako

Muktadha wa taarifa katika lugha ya mama ni bora na inaeleweka kwa urahisi. Kuwa chanzo cha kuaminika cha habari kwa jamii. Ikiwa hakuna mfanyakazi anayezungumza lugha ya asili, juhudi inapaswa kufanywa kupata watu wanaofahamu. Kuna uzalishaji mwingi wa ndani ambao unaweza kushiriki. Mwisho wa mwongozo huu tutashiriki nawe viungo vya tovuti yenye habari ya kuaminika.

Epuka unyanyapaa

Kutokana na asili ya virusi, vyombo vingi vya habari mwanzoni zilitaja kama “ugonjwa wa kichina”, hii ilisababisha ubaguzi wa rangi na ukatili kwa ulimwengu wote unaowaumiza watu wa bara la Asia.



Katika ukanda wetu, jambo kama hilo limetokea kwa sababu uchochezi na ubaguzi umekuwa tishio fiche kwa ndugu zetu wahamiaji na waliosafirishwa kurudi nchi zetu.

Kwa sababu ya hili, tunapendekeza kuwa waangalifu na lugha tunayotumia, epuka matumizi ya kivumishi kuzungumzia utaiifa wa mtu, upendeleo wa chakula, hali ya uhamiaji au hali ya msingi wa kiafya.

Redio kama mtangazaji wa haki za kibinadamu

Redio zinaweza kuunda kampeni za uhamasishaji kuhusu kuheshimu haki za binadamu na kuibua mahali pa mawasiliano (la kukemea ukiukwaji wabinadamu)



Epuka chapisho bila msingi

Hivi sasa kuna udanganyifu mwingi wa kujaribu kupata pesa kutoka kwa watu, au inaweza kutoka kwa watu au vikundi visivyo visumbufu: kwa mfano dawa, mafuta vilainishi au dhana ya muijiza. Ikiwa kuna mtu

anawahakikishia kuwa anaweza kuponya ugonjwa, kama waandishi wa habari tunapaswa kuwauliza maswali, tukitofautisha aina hii ya habari na dawa ya mababu.




Kuripoti chini ya kanuni ya hadhi ya kibinadamu

Ikiwa unamfahamu mtu aliye na dalili au amefariki kutokana na Covid-19, tunapendekeza kushughulikia tatizo kwa kuheshimu familia na mtu husika. Jihadhari na umbali gani unaweza kwenda na mahojiano yako. Jivike viatu vyake katika hali yako hiyo.

Toa taarifa inayotolewa katika jamii zetu na kutoka kwa viongozi wetu Wasilisha hatua ambazo zimechukuliwa kwa ngazi ya kitaifa, kikanda na jamii kutoa maoni juu ya shughuli ambazo zimekataliwa au huziruhusiwi kwa sasa.



Kumbuka redio ni daraja la kuwajulisha watu juu ya dalili muhimu na kujitambulisha na kuruhusu viongozi wa afya kupima walio hatarini na watu wenye dalili. Vipimo ni muhimu sana ili kuzuia kuambukizwa na kulinda afya ya mtu aliyeambukizwa.



Kukuza maadili ya jamii

Kukuza kushirikiana wakati wa kizuizini.

Pendekeza shughuli za kifamilia kwa mfano kufuma, shughuli za shamba, kupika kati ya zingine nyingi.

Pendekeza kuandaa nyumba kwa kugawa kazi za nyumbani ukizingatia usawa wa kijinsia. Kukuza simulizi za kimila mezani au shughuli zingine ambazo hupunguza athari za kisaikolojia ambazo janga hili husababisha.

Kuunda kampeni ya redio dhidi ya dhuluma kwa watoto au wanawake. Sasa kwa kuwa tunawekwa kuzuizini tunapokea ripoti nyingi za dhuluma. Kuwa sauti ya msaada, utulivu na mwamko kwa jamii yako.

Kukuza simulizi za kimila kusambazwa na kushiriki tukijumuika majumbani na shughuli zingine ambazo hupunguza athari za kisaikolojia za janga hili.

Katika maeneo mengi mafunzo ya matandaoni sio njia nzuri ya kushughukia mahitaji ya wanafunzi kutokana na ukosefu wa mtandao na vyanzo vingine. Jiunge katika mundo mpya wa redio kufundisha vijana na watoto kama njia ya kuchangia na kupunguza athari za kufutwa kwa mafunzo na kufungwa kwa shule. Waalike walimu kutoa mafunzo zao kupitia redio.



Wajulishe hadhira kuwa kuweka vizuizi katika maeneo mengine haiashirii kuisha kwa Covid-19. Kupendekeza kuheshimu mapendekezo ya mamlaka ya afya.

Inashauriwa kuzingatia historia chanya na wakati wa jamii kipindi hiki cha ugonjwa huu.

Anza majadaliano mingoni mwa jamii ili kutafakari juu ya mafunzo na jinsi janga hili litakavyotuacha na jinsi ya kuboresha maisha yetu.

Kukuza uhifadhi wa fedha na sio kununua vitu visivyo vya lazima

Waalike wanajamii wazingatie hatua za usafi kwa umakini, pesa haijabainishwa kama njia ya kuambukiza, lakini mzunguko huu unaweza kuwa njia inayoweza kuambukiza.

Kukuza matumizi ya chakula ambacho huimarisha ulinzi wetu na kuunda mpango wa ukombozi wa mapishi ya mababu ambayo hutoa virutubishi muhimu katika maisha yetu iliyoonyeshwa na maisha marefu ya babu zetu.

NI WAPI UPO HATARINI ZAIDI KUAMBUKIZWA VIRUSI





Chanzo kikuu cha habari inayotegemewa

Shirika la afya dunuani

<https://www.who.int/es>

Kurasa maalum za waandishi wa habari kuhusu Covid-19

Mtandao wa waandishi wa habari wa kimataifa

<https://ijnnet.org/en>

Global Investigative Journalism Network

<https://gijn.org/gijn-en-espanol/>

South Africa

<https://sacoronavirus.co.za/>

African Union

<https://africacdc.org/covid-19/>

World Health Organization Africa

<https://www.afro.who.int/health-topics/coronavirus-covid-19>

Cultural  Survival